

Kulikuwa na mzee mmoja aliyeitwa Hagos. Aliishi na wanawe watatu.

Hagos alitaka wanawe wawe na mali baada ya kifo chake. Alitayarisha masanduku matatu.




Hagos alikwenda kwa Haile,
jirani yake, na kumwambia,
“Ninataka wanangu wawe
na mali. Nimeyatayarisha
masanduku matatu.
Ningependa uwapatie
masanduku hayo baada ya
kifo changu.”



Baada ya Hagos kufariki,

Haile aliwaita pamoja wale
ndugu watatu akawaeleza,
“Kabla baba yenu kufariki,
alinipatia haya masanduku
matatu. Kila sanduku lina
jina. Naomba kila mmoja
alichukue sanduku lililo na
jina lake.”




Ndugu wale walichukua kila mmoja sanduku lake kisha wakayafungua.

Sanduku la kwanza lilikuwa na dhahabu. La pili, lilikuwa na udongo. Nalo la tatu lilikuwa na samadi.



Aliyepata dhahabu alifurahi sana. Waliopata udongo na samadi, hawakufurahi. Walianza kugombana na yule aliyepata dhahabu.




Haile aliwaambia, "Ninyi ni
ndugu na hamstahili
kugombana. Hebu
niwapeleke kwa mzee
mwenye busara awashauri."



Haile aliwapeleka ndugu
wale watatu kwa mzee
mwenye busara.

“Habari za asubuhi.
Tumekuja kwako kutafuta
ushauri kuhusu urithi,”
Haile alimweleza yule mzee.



Haile alimwambia yule mzee
mwenye busara kuhusu yale
masanduku matatu ambayo
Hagos aliwaachia wanawe.

“Sasa hawa wawili,
wanagombana na yule
aliyepata sanduku lililokuwa
na dhahabu,” Haile alieleza.




Yule mzee mwenye busara alisizitiza, "Baba yenu alikuwa na sababu ya kuwapatia sanduku ambalo kila mmoja wenu alipata."



Aliendelea kuwaeleza,
“Wewe ulipata dhahabu
kwa sababu babako alitaka
uwe mfanya biashara. Nawe
ulipata udongo kwa sababu
babako alitaka uwe
mkulima.”



"Wewe ulipata samadi kwa sababu babako alitaka uwe mchungaji. Baba yenu alitaka mfanye kazi yenu kulingana na vipaji vyenu," mzee mwenye busara alikamilisha maelezo yake.



Baada ya kusikiliza ushauri wa yule mzee mwenye busara, wale ndugu watatu walikubaliana naye. Kila mmoja wao aliifanya kazi yake tofauti na wakaishi kwa furaha.